



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



## **HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

*Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa*

Simu: +255 262 965 732(Direct line)

Nukushi +255 262 965 732

Barua Pepe: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

Tovuti: [www.sikongedc.go.tz](http://www.sikongedc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

4 MTAA WA BOMANI

S L P 70,

45382 SIKONGE - TABORA

Unapojibu tafadhali taja:

15/8/2022

Kumb.Na.HWS/M.10/15/VOL.VIII/23

### **YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA YA WAKUSANYA MAPATO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kutuma maombi ya nafasi ya kazi za mkataba (wanaweza ongeza) za ukusanyaji wa Mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

#### **1.WAKUSANYA MAPATO (REVENUE COLLECTOR) (Nafasi 12)**

##### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- i) Awe na umri kali ya Miaka 18 hadi 45
- ii) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- iii) Awe amehitimu mafunzo angalau ya cheti katika fani ya uhasibu/fedha/ugavi.
- iv) Awe mwenye nidhamu na mwadilifu katika makusanyo ya Fedha.

##### **MASHARTI YA AJIRA**

- Ajira hii ni ya mkataba

##### **MSHAHARA**

Asilimia (10%) ya makusanyo yanayowasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kila siku


##### **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE**

- Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
- Barua za Mwombaji ziambatanishwe na vivuli vya vyeti vya Elimu,Taaluma,cheti cha kuzaliwa,Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba na picha mbili za rangi (passport size) zilizopigwa hivi karibuni,
- Barua za Maombi ziambatanishwe na maelezo binafsi ya Muombaji (CV) na namba ya simu
- Mwombaji aambatanishe kwenye maombi ya kazi nakala za barua za wadhamini wawili wanaofahamika katika jamii.
- Testimonials, Provisional Results," Statement of Results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (form IV and Form VI Results slips) HAVITAKUBALIWA

- Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na mamlaka husika
- Mwombaji atakayekiuka utaratibu wa maombi haya, hatashughulikiwa ombi lake
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 28/8/2022 saa 9.30 Alasiri, Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta ya Sikonge au yawasilishwe kwenye masjala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sikonge kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P 70  
**SIKONGE**

**NB.** Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri [www.sikongedc.go.tz](http://www.sikongedc.go.tz) na Kwenye Mbao za Matangazo ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge



Seleman M. Pandawe  
Mkurugenzi Mtendaji (W),  
**SIKONGE**



**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**WILAYA - SIKONGE**

**Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022**